SERA FUPI

Ni kwa Namna Gani Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai Inaweza Kujumlisha Utofauti wa Maumbile na Kufungamana na Ahadi za Kimataifa?

Kuhifadhi utofauti wa kimaumbile kwenye viumbe fulani ni muhimu kwa kusaidia viumbe hivyo kukabiliana na mabadiliko ya mazingira ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, viumbe vamizi vya kigeni, uchafuzi wa mazingira, uthabiti wa mfumo wa kiikolojia na urejesho na kusaidia mahitaji ya kijamii. Hapa kuna mapendekezo 10 ya kuhusisha utofauti wa kimaumbile katika ahadi, utekelezi na sera za Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai, huku yakitimiza mahitaji ya uwezo.

Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai wa Kunming-Montreal unatoa motisha na nafasi bora zaidi ya kujumuisha utofauti wa kimaumbile katika sera za kitaifa na kimaeneo. Lengo ‘A’ na azimio la ‘4’ la Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai vinakariri kuwa utofauti wa kimaumbile miongoni na kati ya idadi ya viumbe wa nyumbani na wa mwituni lazima wahifadhiwe, walindwe, watunzwe na warejeshwe. Viashiria vya kuripoti juu ya utofauti wa kimaumbile no mojawapo wa sehemu ya Mfumo wa Uchunguzi, ikiwemo Kichwa Kiashiria A.4. Washirika wa CBD, mashirika ya kitaifa na kimaeneo na mashirika ya uhifadhi yanaalikwa kusasisha na kuunda Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai, kwa kupanga, kutekeleza, kuchunguza na kutathmini hatua za kuafikia malengo na maazimio ya bioanuwai.

Mapendekezo yafuatayo yaliundwa ili kusaidia kuhakikisha kwamba ahadi, hatua na sera katika Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai yanafanikisha kusaidia utofauti wa kimaumbile na kwamba mahitaji ya uwezo yanatimizwa. Mapendekezo yanatokana na kutathmini Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai 21 ulimwenguni kote. Yamewekwa katika makundi matatu maalum jinsi ilivyoanishwa katika CBD/COP/DEC/15/6. Maelezo zaidi na mifano ya kitaifa yaweza kupatikana kwenye msimbo wa QR ulio hapo chini.

Mapendekezo Kumi ya Kuhusisha Utofauti wa Kimaumbile katika Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai

Kuweka malengo ya kitaifa

1. **Husisha wadau wote** ukitumia mbinu ya kuhusisha jamii nzima wakiwemo watu wa asili na jamii za mitaani ili kusbabisha manufaa kwa jamii nzima.
2. **Weka lengo pana la kitaifa likiwa na vipengele na maazimo sawia na yale ya kimataifa**, ikiwemo utofauti wa kimaumbile katika na miongoni mwa watu na kuwe na uwezo wa kubadilika.
3. **Weka malengo ya kitaifa yenye matarajio makuu na maalum,** kama vile kuhusisha sera, utungaji wa sharia, mipango/mikakati ya utofauti wa kimaumbile.
4. **Tambua umuhimu wa utofauti wa kimaumbile katika kuafikia malengo mengine** (Kama vile Lengo 2, 3, 6, 8, 9, 10, 11, 13) kwa kuweka nguvu pamoja, kuchunguza na kuripoti ili kutumia rasilmali na fedha kwa njia iliyo bora zaidi.

Kundeleza hatua, sera na mikakati ili kuafikia malengo, na kuweka bayana mahitaji ya kifedha na uwez

5. **Elezea na ujitolee kwa hatua za kuendeleza na kurejesha utofauti wa kimaumbile** kama vile uhamisho, uanzilishi upya, kurejesha kuunganishwa na makazi, na usimamizi dhabiti wa vitisho**.**
6. **Ainisha mikakati maalum ya sera, mifumo na program iliyopo au ambayo inanuiwa kuwekwa** ili kuwezesha ufanisi chanya wa utofauti wa kimaumbile.
7. **Tambua uwezo au upungufu wa sasa, upungufu wa kifedha na mipango ya kujenga uwezo na mipango ya muda mrefu ya ufadhili** kuendeleza uwezo wa kupata usaidizi wa kujenga uwezo na kushirikiana.

Kuchunguza, kutathmini, kuhakiki kwa kutumia viashiria

8. **Elezea bioanuwai iliopo na aliopangwa kiprogram, kidata, kiuhakiki wa kutathmini** ili kusaidia uchunguzi wa utofauti wa kimaumbile kuwezeshwa kuvuta pamoja na program ziliopo.
9. **Weka mpango wa kuzalisha viashiria na kuripoti** - namna gani na lini data itapatikana, kutumika na kutunzwa kwa muda utakaohitajika; jinsi inavyoambatana na malengo mengine ya kuripoti na mashirika husika.
10. **Tathmini ufahamu uliopo kuhusu utofauti wa kimaumbile kitaifa/kijamii ili kujulisha waunda sera na umma,** ikijumlisha utafiti maalum kuhusu matumizi ya maarifa ya maumbile ili kukuza usimamizi.

THE BIODIVERSITY PLAN
For Life on Earth

THE COALITION FOR CONSERVATION GENETICS

Bofya msimbo wa QR kwa zaidi mapendekezo ya kina

Ni hatua, sera, kukuza uwezo na mikakati gani inayoweza kusaidia utofauti wa kimaumbile? Ni viashiria gani vilivyopo?

HATUA

Kusaidia idadi ndogo kuongezeka, kuwawezesha kuunganika, kutathmini masuala ya afya ya kimaumbile kama vile mseto usiohitajika, kuzaliana, kustawisha uzalishaji wa kiasili na ukulima wa mchanganyiko.

SERA

Ulinzi wa kisheria (k.m. viumbe wa kiasili, viumbe maalum) au uwekezaji maalum wa rasilmali (k.m. kufadhili programu za kuchunguza maumbile, kurejesha makazi, mkusanyiko wa vitu vya kundi/kizazi maalum, au uhifadhi wa jeni.

MIKAKATI AU MIPANGO

Fafanua viumbe mahsusi vinavyopewa kipaumbele katika uchunguzi wa utofauti wa kimaumbile, zingatia utofauti wa kimaumbile katika mipango ya anga, (ikiwemo jinsi inavyoingiliana na mandhari), weka mpango wa kukusanya data, na uhifadhi wa viashiria vya maumbile, weka ratiba ya kukuza uwezo na uchapishe ripoti kuhusu hatua zilizochukuliwa kuwafikia kuhifadhi na kurejesha utofauti wa kimaumbile.

VIASHIRIA

Kiashiria kikuu cha GBF: A.4. Kiwango cha idadi miongoni mwa viumbe walio na idadi dhabiti >500.

Viashiria vya Vipengele na nyongeza: Idadi ya rasilmali za kimaumbile za mimea na wanyama kwa chakula na kilimo iliolindwa katika vifaa vya uhifadhi vya muda wastani au mrefu; idadi ilyohifadhiwa katika viumbe fulani; jinsi viumbe wa mwituni wanakadiriwa kwa utofauti wa kimaumbile; Upana wa uhifadhi wa viumbe walio na thamani ya kitamaduni, kijamii na kiuchumi; kiwango cha viumbe wa kiasili vinavyozingatiwa kuwa karibu kutoweka/kupotea.
**Zingatia: Hakuna mojawapo ya vigezo hivi inayohitaji kipimo cha DNA.*

Mifano ya Kitaifa (Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai)

Hapa chini kuna nukuu kutoka kwa nakala rasimu au zilizokamilika za Mikakati na Mipango Tekelezi ya Bioanuwai au hati kama hizo zikiwa na maandishi yakiashiria umuhimu wa utofauti wa kimaumbile au hatua, sera, matokeo au uchunguzi. Hii sio mifano pekee iliyotambuliwa – tazama nakala iliyochapishwa kwa orodha kamili, kutoka nchi 21. Bonyeza msimbo wa QR hapa chini!

Uswidi (hati ya matumizi ya ndani): Idadi ya viumbe wa asili wa mwituni imehifadhiwa. Kiwango cha yale makundi yaliyo na idadi thabiti kubwa kushinda 500 imeongezeka (malengo na viashiria).

Serbia: Jumuisha ukanda wa ikolojia, kama mojawapo ya sehemu inayotambulika ya Ushirika wa Ulaya wa Mali Asili ili kuzuia kutengwa kwa kimaumbile (ahadi ya kuchukuliwa hatua).

Korea: Utafiti wa majaribio wa kutambua na kuchunguza mara kwa mara utofauti wa kimaumbile wa viumbe walio hatarini, viumbe wanaodhurika, na wale walio na thamani ya juu ya kiuchumi.Tumia matokeo ya uhifadhi wa kundi kwa kila kiumbe na kama thibitisho la kisayansi la kuunga mkono kutambuliwa kwa viumbe muhimu wa kulindwa, kuorodheshwa/kuondolewa kwa orodha kwa viumbe walio hatarini na kuchaguliwa kwa viumbe wa kurejeshwa (kuchunguzwa).

Kambodia: Kukuza na kuendeleza uwezo wa kutumia mbinu za DNA kwa kutambua viumbe na utafiti wa utofauti wa kimaumbile, na kwa uzazi, na mfumo wa idadi, na mfumo wa ikolojia wa afya (ahadi ya hatua na kujenga uwezo).

Ajentina: Kuhifadhi kwa maumbile tofautitofauti kuliko muhimu kwa kuweko kwa idadi ya makundi madogo na kuambatana kwao na kuzambaa katoka maeneo madogo madogo katika nchi nzima ya Ajentina (kauli ya matokeo inahitajika).

SADC: Stawisha na kukuza mashirika ya kimaeneo na kitaifa kwa mipango na mikakati ya utekelezaji na kufuatilia udhabiti wa kuingilia kati kwa minajili ya kuhifadhi utofauti wa kimaumbile (sera na mikakati).

Australia: Ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, viumbe watahitajika kuwa kwa makundi makubwa ya utofauti wa kimaumbile (kauli ya matokeo inahitajika).

kwa msaada zaidi, tembelea CoalitionForConservationGenetics.org

THE BIODIVERSITY PLAN
For Life on Earth

THE COALITION FOR CONSERVATION GENETICS

Bofya msimbo wa QR kwa mapendekezo ya kina na mifano zaidi